WITO>> Wananchi kuzingatia sheria na kanuni za usala

# Madereva 89 wadaiwa kuvunja sheria Pwani

**Na MWAMVUA MWINYI,** *Pwani*

JESHI la Polisi, Kikosi cha Usalama Barabarani, limewakamata madereva 89 mkoani Pwani, kwa tuhuma za uvunjifu wa sheria za usalama barabarani.

Madereva hao wamekamatwa katika operesheni maalumu iliyofanyika kuanzia Julai 12, mwaka huu, Barabara Kuu ya Morogoro.

Akizungumza katika operesheni hiyo, Ofisa Mnadhimu wa Kikosi cha Usalama Barabarani Tanzania, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi, Butusiyo Mwambelo, aliwaagiza askari wa kikosi hicho, Mkoa wa Pwani kuchukua hatua dhidi ya madereva wanaokiuka sheria, bila uoga.

"Madereva wanaokiuka sheria ni lazima wakamatwe na kuadhibiwa. Waelimishwe wao na abiria waliopo katika vyombo vyao vya usafiri, kupunguza ajali ambazo nyingi husababishwa na uzembe wa binadamu," alisema.

Kwa upande wake, Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani Mkoa wa Pwani, Mrakibu Mwandamizi wa Polisi, Edson Mwakihaba aliwaasa madereva wa mabasi ya abiria na malori kutii sheria, bila shuruti.

"Madereva mnapaswa kutii sheria, bila kulazimishwa na wale wakaidi ninataka kuwaeleza wazi hatua kali zitachukuliwa, ikiwemo kufungiwa leseni zao," alisema.

Alitoa wito kwa watumiaji wa barabara kuzingatia sheria na kanuni za usalama barabarani, kwa usalama wa maisha yao na ya wengine.

Operesheni hiyo imelenga kukagua makosa ya usalama barabarani yakiwemo kupakia abiria kupita kiasi, kutokuwa na vibali vya VTS, kupita magari mengine bila kuchukua tahadhari na kubeba abiria katika magari yanayoelekea nje ya nchi (IT).

Uhuru. Alhamisi Julai 17, 2025 Pg 16

# Dereva pikipiki anaswa akiendesha gari la abiria

**Na WARIOBA IGOMBE**, *Morogoro*

POLISI mkoani Morogoro, wamefanya operesheni ya kushtukiza ya ukaguzi wa magari ya mizigo na abiria Barabara Morogoro-Dodoma na kumbaini dereva mwenye leseni ya pikipiki akiendesha gari la abiria.

Akizungumza baada ya ukaguzi huo, uliofanyika juzi, Kamanda wa Polisi, Mkoa wa Morogoro, SACP Alex Mkama, alisema wamebaini zaidi ya magari 10 ya mizigo na abiria yana dosari mbalimbali, ikiwemo baadhi ya madereva kutokuwa na sifa.

"Ukaguzi huu tumeufanya kwa kushtukiza na kubaini kuna dereva ana leseni ya kuendesha pikipiki na anaitumia kuendesha gari la abiria, tumemkamata. Pia, baadhi ya magari ni mabovu na matairi yake yamechakaa,"alisema Mkama.

Mkama alisema operesheni imewezesha kukamatwa kwa magari zaidi ya 10 yakiwa na makosa mbalimbali hatarishi, yakiwemo matairi kuisha na mengine yakiwa hayana nati katika lingi za matairi, kitu ambacho ni hatari.

Alisema ajali nyingi zimesababishwa na uzembe wa madereva, hivyo kitendo cha kuwakamata na magari yao, kutasaidia kuwakumbusha wajibu wao, hivyo kupunguza ajali za barabarani mkoani humo.

Aliahidi kuwa, ukaguzi utakuwa endelevu mkoani humo na kwamba jeshi hilo halitamfumbia macho dereva atakayebainika kuvunja sheria za usalama barabarani na kuwataka kuzingatia sheria, kuepuka mkono wa sheria.

Baadhi ya madereva ambao magari yao yalikamatwa walikiri makosa na kusema kitendo hicho siyo cha uonevu kwani kimelenga kupunguza ajali ambazo zimegharimu maisha ya watu.

Christopher Iga alikiri kosa alilokutwa nalo na kusema ukaguzi huo ni mzuri, unawatoa usingizini na kuwakumbusha namna ya kutekeleza majukumu yao kwa ufasaha zaidi kwa kuzingatia sheria za usalama barabarani.

Mwenyekiti wa Balozi wa Usalama Barabarani, mkoani Morogoro, Steven Masoni, alisema operesheni hiyo imelenga kupunguza ajali za barabarani ambazo mara kwa mara zimeripotiwa mkoani humo.

Alilipongeza jeshi hilo kwa kuendesha ukaguzi huo, utakaosaidia kupunguza ajali za barabarani kwa kuwa madereva watafanya kazi kwa ufasaha, wakiogopa kukamatwa.

**LENGO**

**OPERESHENI**

Mwenyekiti wa Balozi wa Usalama Barabarani, mkoani Morogoro, Steven Masoni, alisema operesheni hiyo imelenga kupunguza ajali za barabarani ambazo mara kwa mara zimeripotiwa mkoani humo.

CamScanner